# CLASS 5 END TERM 2 2020

# KISWAHILI

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.*

Kenya ni mojawapo ya nchi___1___Afrika Mashariki Afrika Mashariki___2___nchi tano; nazo ni Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda na Urundi.

Nchi___3___ya Kenya imebarikiwa sana___4___na maliasili tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Maliasili___5___ni milima, misitu, mito, bahari na wanyamapori kutaja tu machache.

___6___mlima Kenya kwani___7___mlima___8___kwa___9___barani Afrika. Milima, misitu na mito na bahari hutupa mandhari ya kuvutia.___10___iliyo___11___mlima Kenya huvutia kutazama. Nao mchanga ___12___ulio kwenye fuo___13___za bahari huwavutia watalii kutoka pembe zote za dunia. Lakini rasilimali yetu kubwa ni wanyamapori___14___. Hao ndio kivutio___15___sana cha watalii.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** ya | **B.** wa | **C.** la | **D.** za |
| **2.** | **A.** iko | **B.** ina | **C.** iko na | **D.** zina |
| **3.** | **A.** wetu | **B.** letu | **C.** yetu | **D.** chetu |
| **4.** | **A.** kuwa | **B.** kwa | **C.** kua | **D.** na |
| **5.** | **A.** hiyo | **B.** hilo | **C.** hayo | **D.** hizo |
| **6.** | **A.** Tunafurahia | **B.** Tunaringia | **C.** Tunasherehekea | **D.** Tunajivunia |
| **7.** | **A.** ndio | **B.** ndiyo | **C.** ndilo | **D.** ndiwo |
| **8.** | **A.** wawili | **B.** wa pili | **C.** wa mbili | **D.** wapili |
| **9.** | **A.** ukubwa | **B.** unene | **C.** upana | **D.** urefu |
| **10.** | **A.** Ukungu | **B.** Theluji | **C.** Barafu | **D.** Baridi |
| **11.** | **A.** juu ya | **B.** kando ya | **C.** chini ya | **D.** mbele ya |
| **12.** | **A.** mchafu | **B.** msafi | **C.** safi | **D.** chafu |
| **13.** | **A.** wetu | **B.** zetu | **C.** yetu | **D.** letu |
| **14.** | **A.** wao | **B.** wake | **C.** wako | **D.** wetu |
| **15.** | **A.** kikubwa | **B.** mkubwa | **C.** kubwa | **D.** likubwa |

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Kamilisha sentensi kwa kiunganishi sahihi.
*Huwezi kununua ________ pesa.*
A. na B. wala
C. bila D. bali

**17.** Andika sentensi ifuatayo katika wakati wa mazoea.
*Mimi ninakula wali*
A. Mimi hula wali.
B. Mimi nilikula wali.
C. Mimi nitakula wali.
D. Mimi nakulanga wali.

**18.** **Kamilisha kwa kivumishi sahihi**
*Chumbani mlikuwa na watu __________*
A. matatu. B. tatu.
C. mitatu. D. watatu.

**19.** Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:
Tunda lote limeoza
A. Tunda zote zimeoza.
B. Matunda zote zomeoza.
C. Matunda yote yameoza.
D. Matunda yote imeoza.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

20. Ni sentensi gani imetumia 'amba' kwa usahihi?
A. Mtu ambaye atashinda atatuzwa.
B. Kalamu ambayo iliyopotea imepatikana.
C. Fundi amerekebisha meza ambayo iliyovunjika.
D. Maji ambayo yaliyomwagika yamepanguswa.

21. Andika nambari kwa maneno
*Amenunua maembe (8)*
A. minane. B. manane.
C. nane. D. wanane.

22. Tumia kiulizi kwa usahihi:
Miti iliyopandwa ni _________?
A. upi B. zipi
C. vipi D. ipi

23. Neno choo liko katika ngeli gani?
A. I - I B. KI - VI
C. I - ZI D. LI-YA

24. Tumia kihusishi sahihi
*Waliomba _______ kuanza kula.*
A. baada ya B. mbele ya
C. kabla ya D. nyuma ya

25. Ni sentensi ipi inaonyesha -ki- ya udogo
A. Kijumba chake kimebomoka.
B. Kichwa chake kinauma.
C. Chumba hiki ni kichafu.
D. Chakula changu kimeharibikia.

26. Kamilisha kwa kivumishi cha idadi sahihi
Alikuwa wa___(1)___kuondoka.
A. moja B. mwanza
C. mmoja D. kwanza

27. **Kamilisha methali ifuatayo**
*Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na*
__________
A. babaye. B. ulimwengu.
C. dunia. D. mwalimu.

28. Dada ya mama wako utamwitaje?
A. Nyanya. B. Shangazi.
C. Halati. D. Wifi.

29. Ni neno gani lililo tofauti na mengine?
A. Sindano. B. Bandeji.
C. Randa. D. Dawa.

30. Kikembe cha ndege huitwa _________
A. kifaranga. B. kinda.
C. nyuni. D. kiyoyo.

<u>*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*</u>

Salamu zilikuwa na umuhimu mkubwa sana kulingana na utamaduni wetu wa kiafrika. Watu waliamkuana ili kujuliana hali. Salamu zilikuwa ni njia moja ya kuonyesha adabu na heshima. Aliyesalimia alionekana kuwa mtu mwenye adabu na heshima; naye aliyesalimiwa alijisikia kuwa ameheshimika.

Salamu vilevile zilionekana kama ishara ya amani. Iwapo mtu angemsalimia mwenzake, naye mwenzake aitikie salamu hizo, basi ilionyesha kuwa kulikuwa na amani baina yao. Lakini kama anayesalimiwa angenyamaza, asiitikie, basi ilionyesha kuwa kulikuwa na jambo au uhasama baina yao. Kukosa kuitikia salamu pia kungemtia mtu matatani kwani kungewafanya wenyeji wamshukuru mtu huyo kuwa haifahamu lugha yao na hivyo kumdhania kuwa adui.

Lakini siku hizi mambo yamebadilika kabisa. Watu wengi hawathamini salamu hata kidogo. Hii ni kwa sababu hakuna mtu anayejali hali ya mwengine; kila mtu anajishughulisha na maisha yake tu. Ule utu na udugu wa kiafrika tuliokuwa nao umetutoka kabisa. Pengine mabadiliko haya yamesababishwa na hali ya maisha ya kisasa; ama pengine ni uigaji wa tamaduni za kigeni; sina hakika sana.

Katika juhudi za kujaribu kurekebisha mambo, wizara ya elimu imejaribu kutilia mkazo mafunzo kuhusu maamkuzi na adabu. Hii inadhihirika katika silabasi na vitabu vya ziada vya kiswahili. Silabasi za madarasa yote na vitabu vyote vya ziada huanza na somo: 'Mamkuzi na Adabu'.

Mbali na kuzisoma salamu tu kama somo walimu huwahimiza wanafunzi kuliweka somo hilo katika matendo shuleni, nyumbani na mahali popote. Mwalimu anapoingia darasani wanafunzi husimama kwa heshima na kumpa salamu" "Shikamoo mwalimu". Naye mwalimu hujibu: "Marahaba wanafunzi" Wakati mwingine mwalimu ndiye huwa wa kwanza kuwasalimia wanafunzi: "Hamjambo wanafunzi?" Nao hujibu kwa heshima: "Hatujambo mwalimu, shikamoo".

Kusalimiana kabla ya somo kuanza huleta hali ya amani baina ya mwalimu na wanafunzi na kulifanya somo kuendelea vizuri. Hii amani inayoletwa na salamu haifai tu kuishia shuleni bali yafaa pia kufika nyumbani. Hii ni kumaanisha kuwa salamu pia ni za muhimu kati ya watoto na wazazi wao, kwani kila tabia njema yafaa kuanzia nyumbani.

**31.** Salamu zilikuwa njia moja ya kuonyesha __________
A. amani na upendo. B. amani na umoja.
C. utiifu na heshima. D. adabu na heshima.

**32.** Aliyesalimiwa alijisikia kuwa ____________
A. ameheshimiwa. B. amedharauliwa.
C. amependwa. D. amefarijiwa.

**33.** Kukosa kuitikia salamu kulionyesha yafuatayo isipokuwa
A. kulikuwa na jambo.
B. wenyeji wangemheshimu mtu huyo.
C. kulikuwa na uhasama.
D. wenyeji wangemshuku mtu huyo.

**34.** Mambo yafuatayo yamebadilika kabisa siku hizi isipokuwa
A. watu wengi wanapenda salamu.
B. watu wengi hawathamini salamu.
C. hakuna mtu anayejali hali ya mwengine.
D. kila mtu anajishughulisha na maisha yake.

**35.** Kulingana na mwandishi, ni nini kinachosababisha mabadiliko haya?
A. Njia za mawasiliano ya kisasa.
B. Mali ya maisha ya kisasa.
C. Uigaji wa tamaduni za kigeni.
D. Mwandishi hana hakika sana.

**36.** Ili kujaribu kurekebisha mambo, wizara ya elimu imejaribu kutilia mkazo mafunzo kuhusu
A. sayansi na teknolojia.
B. amani na utangamano.
C. maamkuzi na adabu.
D. amani na umoja.

**37.** Walimu huwahimiza wanafunzi kuliweka somo hili katika matendo mahali gani kulingana na hadithi?
A. Shuleni tu.
B. Mahali popote.
C. Nyumbani tu.
D. Shuleni na nyumbani tu.

**38.** Taja salamu zilizotumika kwenye hadithi __________
A. shikamoo, hamjambo.
B. sabalkheri, habari.
C. sabalkheri, masalkheri.
D. shikamoo, mwambaje.

**39.** Kusalimiana kabla ya somo kuanza huleta nini baina ya mwalimu na wanafunzi?
A. Hali ya uhasama.
B. Hali ya maelewano.
C. Hali ya amani.
D. Hali ya masikizano.

**40.** Kulingana na mwandishi kila tabia njema yafaa kuanzia
A. shuleni. B. darasani.
C. kanisani. D. nyumbani.

*<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>*

Waridi alikuwa mtoto wa pekee kwa wazazi wake; na kama jina lake linavyoashiria, alikuwa mrembo kwelikweli. Pengine urembo wake ndio uliofanya wazazi wake wakampa jina Waridi.

Wazazi wake walimlea kwa kumdekeza. Walimvika upendo kama vazi. Hawakutaka kusikia mwana wao wa pekee akilia. Chochote alichowaomba walimpa. Tangu kuzaliwa kwake, wazazi wake walimwajiri yaya wa kumlea. Yaya huyu alimtunza hadi alipotimu umri wa kwenda shule ya chekechea, akawacha kazi.

Haikupita muda mrefu wazazi wa Waridi waliajiri mfanyakazi wa nyumbani. Walifanya hivyo kwa sababu wote walikuwa wameajiriwa na binti yao alihitaji mtu wa kumtunza wakiwa kazini. Hilo lilionekana wazo la busara kwa watu walioajiriwa kama wao. Tatizo walilokuwa nalo wazazi wa Waridi ni kuwa hawakutaka binti yao afanye kazi yoyote. Kwa nini afanye kazi na kuna mfanyakazi wa nyumbani ambaye analipwa mshahara? Wakati wote alipokuwa shule ya msingi, Waridi hakujua kufua nguo, kupiga pasi, kupika chakula, kuosha vyombo, hata kufagia nyumba. Shuleni aliwaringia wenzake kuwa kwao wana mfanyikazi na yeye anakaa kama malkia.

Baada ya kufanya mtihani wa darasa la nane alifaulu vizuri na kujiunga na mojawapo ya shule bora za kitaifa. Alidhani kuwa mambo yangekuwa kama kawaida kumbe alikuwa amekosea. Sheria za shule zilikuwa kali na nidhamu ilikuwa ya hali ya juu. Makosa kidogo yangefanya mwanafunzi aadhibiwe vikali ama hata afukuzwe shule.

Mbali na nidhamu ya hali ya juu, mwanafunzi alitakikana adumishe usafi wa mwili, mavazi na mazingira. Hii inamaanisha kuwa mwanafunzi alitakikana afue mara kwa mara, afagie na asafishe bweni na darasa. Hii ilionekana kama utumwa kwa Wardi kwani hakuwa amezoea kazi za aina hii. Wazazi hawakuelewa ni kwa nini binti yao afanyishwe kazi na ilhali kuna wafanyakazi wanaolipwa na serikali. Hata hivyo ilibidi Waridi avumilie ili apate elimu bora, kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame.

Alipomaliza kidato cha nne Waridi alijipata akisomea kazi ya usimamizi wa hoteli. Alishangaa kuona kuwa mambo aliyokuwa akichukia kufanya ndiyo yaliyotiliwa mkazo. Usafi ulikuwa ni ***lazima kama ibada hotelini***. Usafi jikoni, usafi kwenye vyumba vya kulala na usafi wa mazingira jumla. Mbali na usafi, ukarimu na ushirikiano mzuri na wafanyikazi wote ulihitajika.

Kutokana na aliyopitia Waridi alitambua kuwa shule ya maisha huanzia nyumbani; na mzazi huchangia pakubwa katika kufaulu au kutofaulu kwa mtoto maishani. Alishukuru pia kwa nidhamu aliyopitia katika shule ya upili kwani ndiyo iliyobadilisha mtazamo wake wa maisha. Kweli mtoto umleavyo ndivyo akuavyo na samaki mkunje angali mbichi.

---

**41.** Mwandishi anadhani kuwa kilichowafanya wazazi wa Waridi wampe jina hilo kilikuwa ni

A. urembo wake. B. unyenyekevu wake.
C. upole wake. D. utiifu wake.

**42.** Wazazi wa Waridi walimlea kwa njia zifuatazo isipokuwa

A. kumdekeza. B. kumpenda.
C. kumchapa. D. kumpa chochote.

**43.** Kwa nini wazazi wa Waridi waliajiri mfanyakazi?

A. Hawakutaka kumtunza.
B. Alikuwa mtukutu.
C. Waridi aliwaomba.
D. Walikuwa wameajiriwa.

**44.** Wazazi wa Waridi walikuwa na tatizo gani kuhusu binti yao? Hawakutaka

A. aende shuleni.
B. afanye kazi yoyote.
C. kumwacha peke yake.
D. kumnunulia chochote.

**45.** Ni kazi gani kati ya zile Waridi hakujua kufanya haikutajwa?

A. Kulima. B. Kufua nguo.
C. Kupiga pasi. D. Kupika chakula.

**46.** Ni jambo gani si kweli kuhusu shule ya upili?

A. Sheria zilikuwa kali.
B. Nidhamu ya hali ya juu.
C. Kudekezwa kwa wafanyakazi.
D. Kufukuzwa shule.

**47.** Mbali na nidhamu ya hali ya juu ni jambo gani jingine mwanafunzi alitakikana adumishe?

A. Amani. B. Urembo.
C. Uzembe. D. Usafi.

**48.** Maneno 'lazima kama ibaada' yamepigwa mstari. Maneno haya ni mfano wa

A. vitendawili. B. tashbihi.
C. methali. D. tanakali za sauti.

**49.** Waridi alitambua kuwa shule ya maisha huanzia __________

A. shuleni. B. gerezani.
C. nyumbani. D. hotelini.

**50.** 'Samaki mkunje angali mbichi' Ni methali gani nyingine yenye maana sawa na hii?

A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
B. Udongo upate ungali maji.
C. Mcha mwana kulia hulia yeye.
D. Aliye juu mngoje chini.